



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA



Kumb Na.KMC/F.20/27

20/03/2025

**YAH: TANGAZO LA MKOPO WA SERIKALI (ADVANCE LOAN) UNAOTOLEWA NA
HAZINA KWA WATUMISHI WA UMMA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama inapenda kuwataarifu Watumishi wote wa Manispaa ya Kahama kuwa imepata mgao wa Fedha kutoka kwa Katibu Mkuu wizara ya Fedha kiasi cha Tsh. **400, 000,000/=** (Milioni Mia Nne), Kwaajili ya Mkopo usio na Riba kwa Watumishi wa Umma wenye sifa waweze kukopa.

Mkopo husika utaombwa kwa njia ya mtandao (online loan Application) tofauti na utaratibu ambao ulikuwa unatumika awali na pia mkopo huu hautaombwa kwa njia ya ESS (Watumishi Portal).

Mtumishi atatakiwa kujisajili kupitia anuani ya mtandao (online link address) maalumu ambayo ni <https://als.muse.go.tz>

Mkopo utakaotolewa ni pamoja na
-Mkopo wa Fedha Tslim,
-Mkopo wa magari/pikipiki chakavu za Serikali.

Mambo ya Kuzingatia;

- Mkopaji awe ni Mtumishi wa Umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.
- Salio la 1/3 ya mshahara
- Mkopaji atalipa 'Service Charge' (Gharama za kuandaa Mkopo) 3% na 'Protection Fund' (Ulinzi wa mkopo) 1% kutoka kwenye Mkopo huo.
- Hautakopeshwa mkopo mwingine kabla ya kurejesha mkopo wa awali.
- Utaruhusiwa kufuta mkopo wako wakati wowote kwa utaratibu uliotolewa.

Hivyo Watumishi wenye sifa wanaotaka kukopa wanatakiwa kujisajili na kuwasilisha maombi yao mwisho tarehe **03/04/2025**.

NB: Mkopo huu haununui deni kutoka Benki au Taasisi nyingine ya Fedha.

Nawasilisha,


Dkt B.H. Msumi
**KAIMU MKURUGENZI
MANISPAA YA KAHAMA**

**MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA**